# Minister: Mark all protected marine areas

By Alfred Zacharia
@azacharia3
azacharia@tz.nationmedia.com

**Dar es Salaam.** The Minister for Livestock and Fisheries, Mr Mashimba Ndaki, has ordered the Tanzania Marine Parks and Reserves Unit (MPRU) to identify and mark all marine protected areas in the Indian Ocean before the end of August, this year, in attempt to avoid conflicts with fishermen.

He issued the order on Tuesday when speaking to residents of Jibondo Ward in Mafia, who complained of being fined for allegedly fishing in the restrictive areas.

Accompanied by his deputy minister, Ms Pauline Gekul, Mr Ndaki asked the fishermen to demand receipt generated from the electronic fiscal devices (EFD) when fined for various offenses.

"Let us make the boundaries of the reserved areas clear so that fishermen can understand them. I want this to be done until August 2021," said Mr Ndaki, demanding involvement of the residents and their leaders during the marking.

Mr Ndaki also called for a one-month research on the fishing nets used by the fishermen and suggest the best alternatives.

Scanned with CamScanner

# TALIRI tells poultry farmers to embark on commercial farming

By Guardian Correspondent, Dodoma

TANZANIA Livestock Research Institute (TALIRI) has urged poultry farmers to change their minds and embark on commercial farming for them to increase productivity and income.

Aluna Chawala, TARILI acting director in Mpwapwa, Dodoma made the call here when the deputy minister for Livestock and Fisheries Pauline Gekul met with the farmers to discuss several issues facing the sector.

According to him, farmers have to adhere to the experts' instructions and embark on smart chicken farming if they want to obtain profits in the business.

He said the country need for more people to embark on chicken farming as it is among the area which its potential is yet to be fully exploited.

Chawala said that the government has introduced new system to start selling the chickens per kilogramme and not by estimations as it was in previous years so as to enable farmers benefit from the trade.

"I urge poultry farmers to invest in modern farming methods so as to keep up with the modern market; this will also help them grow economically. Taking good care of the chickens will also improve their weight thus selling at a good price," he said.

He said the government wants to see its people, waking up and start thinking on doing their income generating activities including poultry farming in a modern way so as to support and maintain the country middle income status.


"So it is high time now for poultry farmers should change their minds and embark on commercial poultry farming so as to benefit more and improve their lives," he said.

He also urged farmers to remember conducting vaccination appropriately as to guarantee safety of the chickens from diseases.

The expert further said if farmers will apply vaccination as advised by experts, they will greatly reduce deaths of mature chickens something which will also increase income.

Scanned with CamScanner

# Gekul amsimamisha kazi mkaguzi wa mifugo



**Na Mwandishi Maalumu, Pwani**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amemsimamisha kazi Mkuu wa Kituo cha Ukaguzi wa Mifugo cha Ruvu Darajani, Gabriel Lyakurwa kwa tuhuma za kutorosha mifugo na kusababisha upotevu wa mapato ya serikali.

Pia amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo kuwachukulia hatua watumishi walio chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambao walikuwa wanashirikiana na mkuu huyo wa kituo katika kutenda uhalifu.

Gekul alitoa maamuzi hayo baada ya mkuu huyo wa Mkoa wa Pwani kuibua tuhuma hizo katika ziara yake aliyoifanya kwenye kituo hicho kilichopo Ruvu Darajani, Wilayani Bagamoyo juzi.

Ndikilo alisema uchunguzi alioufanya umebaini kuwa mkuu wa kituo hicho amekuwa akishirikiana na wenzake wasio waaminifu kutorosha mifugo inayopelekwa katika kituo hicho kwa ajili ya kukaguliwa kabla ya kuruhusiwa kupelekwa katika maeneo mengine ya minada.

"Nimefanya uchunguzi wa kina na kugundua kuwa utoroshaji huu unahusisha mtandao wa watu wengi wakiwemo baadhi ya wananchi, wafanyabiashara na watumishi wa serikali..."

Kwa mfano tarehe 17 mwezi huu wa pili kuna magari matano yalileta ng'ombe katika kituo hiki kwa ajili ya kukaguliwa lakini ni gari moja tu lililokwenda Dar es Salaam kama kawaida huku mengine yaliyobaki yakichepushwa na mifugo ilipelekwa Kisarawe, Kibaha na Kijiji cha Kidogozero ," alisema.

Kutokana na tuhuma hizo, Gekul alitoa maagizo hayo ya kusimamishwa kazi mkuu huyo wa kituo huku akisema Wizara itaunda tume maalumu kwa ajili ya kwenda kuchunguza tuhuma hizo ikiwemo kupitia mahesabu yote ili kubaini ni kwa kiasi gani mapato ya serikali yamepotea.

"Hatuwezi kucheza na maduhuli ya serikali, haiwezekani tuwe na ng'ombe zaidi ya milioni 33 lakini mchango wa sekta ya mifugo katika pato la taifa hauzidi asilimia saba, ni kwa sababu ya michezo kama hii, hatutakubali, tutakwenda kukagua katika maeneo yote ya minada," alisema.

Naye, Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete alisema kuwa katika jambo ambalo wamekuwa wakilisemea sana ni kituo hicho kukithiri kwa vitendo vya ubadhirifu ambavyo vimekuwa vikichangia Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kupoteza mapato.

Scanned with CamScanner

# Gekul amsimamisha kazi Mkuu Kituo cha Ukaguzi Mifugo

**Na Mbaraka Kambona, Pwani**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amemsimamisha kazi Mkuu wa Kituo cha Ukaguzi wa Mifugo cha Ruvu Darajani, Gabriel Lyakurwa kwa madai ya kutorosha mifugo na kusababisha upotevu wa mapato ya serikali.

Pia aliimuagiza Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo kuwachukulia hatua watumishi waliochini ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, ambao walikuwa wanashirikiana na mkuu huyo wa kituo.

Gekul alitoa maamuzi hayo baada ya Mkuu huyo wa Mkoa wa Pwani, kuibua tuhuma hizo katika ziara yake aliyoifanya kwenye kituo hicho kilichopo Ruvu Darajani wilayani Bagamoyo juzi.

Mhandisi Ndikilo alisema, uchunguzi alioufanya umebaini kuwa Mkuu wa kituo hicho amekuwa akishirikiana na wenzake wasiowaaminifu kutorosha mifugo inayopelekwa katika kituo hicho kwa ajili ya kukaguliwa, kabla ya kuruhusiwa kupelekwa katika maeneo mengine ya minada.

Naibu Waziri; "Nimefanya uchunguzi wa kina na kugundua kuwa utoroshaji huu unahusisha mtandao wa watu wengi wakiwemo baadhi ya wananchi, wafanyabiashara na watumishi wa serikali.

"Kwa mfano tarehe 17 mwezi huu wa pili, kuna magari matano yalileta ng'ombe katika kituo hiki kwa ajili ya kukaguliwa, lakini ni gari moja tu lililokwenda Dar es Salaam kama kawaida ilivyo, huku mengine yaliyobaki yakichepushwa na mifugo ilipelekwa Kisarawe, Kibaha na Kijiji cha Kidogozero kinyemela," alisema Mhandisi Ndikilo

Baada ya tuhuma hizo, Naibu Waziri Gekul alitoa maagizo hayo ya kusimamishwa kazi mkuu huyo wa kituo huku akisema, Wizara itaunda tume maalumu kwa ajili ya kwenda kuchunguza tuhuma hizo ikiwemo kupitia mahesabu yote, ili kubaini ni kwa kiasi gani mapato ya serikali yamepotea na wale wote watakaoonekana kuhusika katika upotevu huo watachukuliwa hatua kali.

"Hatuwezi kucheza na maduhuli ya serikali, haiwezekani tuwe na ng'ombe zaidi ya milioni 33 lakini mchango wa sekta ya mifugo katika pato la taifa hauzidi asilimia saba ni kwa sababu ya michezo kama hii, hatutakubali, na tutakwenda kukagua katika maeneo yote ya minada," alisema.

Naye Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete alisema katika jambo ambalo wamekuwa wakilisemea sana ni kituo hicho, kukithiri kwa vitendo vya ubadhirifu ambavyo vimekuwa vikichangia Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kupoteza mapato.

Ridhiwani alimuomba Naibu Waziri huyo, kuhakikisha anachukua hatua madhubuti za kudhibiti vitendo hivyo vya ubadhirifu, ikiwemo kuondoa mtandao wote wa wahalifu ili halmashauri iweze kupata mapato yanayostahili



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (katikati) akijadiliana jambo na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo (kushoto) na Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete (kulia) alipofanya ziara ya kukagua Kituo cha Ukaguzi wa Mifugo cha Ruvu Darajani kilichopo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani juzi.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

